

**KANISA KATOLIKI JIMBO KUU LA DAR ES SALAAM
PAROKIA YA MT. MARIA DE MATTIAS – MIVUMONI
DAR ES SALAAM**

**MATANGAZO YA SHEREHE YA BWANA WETU YESU KRISTO MFALME
MWAKA C TAREHE 20 NOVEMBA, 2022.**

Kristo...

MCHANGO WA PILI

Kwa ajili ya **UJENZI WA OFISI**. Jumuiya iandae vyombo, kwaya mtuongoze kwa wimbo.

NDOA

Bw. Yuda Thadeus Lello mtoto wa Claudi John na Gratiana Peter na Bi. Liliana Mkabahati mtoto wa Silvani Gregory na Pudenciana Msuri.

Tangazo la Pili.

Anayejua kizuizi cha Tangazo hili atoe taarifa ofisi ya mapadre.

TANGAZO KWA WASEMINARI WA ZAMANI

Mhashamu Jude Thaddaeus Ruwa'ichi anawaalika Waumini walei wote ambao walisoma na kupata malezi katika Seminary mbalimbali na wanaishi DSM kushiriki Misa maalumu ya kumshukuru Mungu kwa malezi ambayo waliyapata Seminarini. Baada ya Misa Askofu atapenda kuwa na mazungumzo na wote watakaoshiriki. Mahali na tarehe itakapofanyika Misa itatangazwa baada ya zoezi la kujiandikisha kukamilika. Washiriki ni wale tu ambao wamesoma au wamemaliza seminari ndogo kabla yam waka 2010 na ambao wamemaliza seminari kubwa kabla yam waka 2015.ili kujiandikisha fika ofisi ya H/ Walei Parokia.

UTOTO

Kutakuwa na Ibada ya kuhitimisha Jubilei ya miaka 25 tangu kuanzishwa kwa Utoto Mtakatifu itakayofanyika Jumamosi ijayo tarehe 26/11/2022. Kutakuwa na Ibada ya Misa Takatifu ikifuatiwa na michezo mbalimbali itakayoandaliwa kikanda na baadae kutakuwa na chakula cha Pamoja kwa Watoto na walezi wao hapa Parokiani. Washindi watapewa zawadi. Tunaomba ushirikiano kutoka kwa wazazi.

MAVUNO

Tunawshukuru wana Parokia wote kwa majitoleo ya Tegemeza Jimbo. Tulipeleka kiasi cha shilingi 26,778,000. Mungu awabariki kwa majitoleo hayo.

SHUKRANI

Uongozi wa WAWATA Parokia unatoa shukrani za dhati kwa Baba Paroko, Kamati Tendaji na wanaparokia kwa ushirikiano walioonyesha kwenye siku ya WAWATA iliofanyika Dominika iliopita. Mungu awabariki sana.

UJENZI WA OFISI

Plasta imemalizika, sasa kazi iko kwenye hatua ya kuweka floor.

HUDUMA KANISANI

Leo tunahudumiwa naJumuiya ya Mt. Luka Mwinjili Dominika ijayo tutahudumiwa na Jumuiya ya Marko Mwinjili Wakati huohuo Jumuiya ya Mt. Yosefu Mfanyakazi wajiandae.

MAUZO

Gazeti la Tumaini letu linapatikana kwenye duka la WAWATA kwa shilingi 1,000 tu.Jipatie nakala yako ilio sheheni habari kemkem

TUSIKILIZE SADAKA NA MATOLEO MENGINE DOMINIKA ILIYOPITA.